# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI ZA SERIKALI

**Juni, 2024**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu;**

**Mkuu wa Shule: 0717404471/0757246378**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0712999822**

**Matron: 0682546688/0673446103**

**Shule ya Sekondari:Mahiwa**

**S.L.P.129 Mtama**

**Lindi**

**Tarehe .08/05/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**:** **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAHIWA HALMASHAURI YA MTAMA MKOA WA LINDI MWAKA 2024**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya ___________________

Shule ya Sekondari Mahiwa ipo umbali wa kilometa 82 kutoka makao Makuu ya Mkoa wa Lindi.Pia ipo kilometa 12 kutoka makao makuu ya Halmashauri ya mtama Usafiri wa basi kutoka Dar es salaam unapatikana katika kituo cha mabasi Mbezi/Temeke/Mbagala mpaka **kituo cha mabasi Nyangao** na Kutoka Lindi mjini kuelekea Masasi. Mwanafunzi anatakiwa kushuka **kituo cha mabasi Nyangao** na kukodi pikipiki ni shilingi 2000/=, kwa bajaji shilingi 5,000/= Kuelekea Shule ilipo Umbali wa kilometa nne (4) kutoka Nyangao.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 01/07/2024 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 30/06/2024. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 14/07/2024

## 1. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 1.1 Sare za Shule

(a) WASICHANA

- Sketi ndefu mbili rangi ya kijivu cha kupauka zenye V mbele isiyobana na isiwe na mpasuo
- Shati mbili nyeupe mikono mifupi aina ya Tomato (wasiovaa Hijabu,) Na kwa wanaovaa hijabu ni NUSU KANZU. Na shungi nyeupe ndefu yenye kustiri mikono na kifua)
- Sweater 1 kwa ajili ya kujikinga na baridi(Rangi **kijivu**)

**Nguo za kushindia na shamba dress na Michezo**

- Sketi nyeusi mbili na Tshirti mbili cream zenye nembo ya shule(Tshirt zinapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh 15,000/= kwa moja) Kwa wanaovaa hijabu,hijabu iwe rangi ya zambarau kwa ajili ya kazi za shamba
- Track suit rangi ya kijivu kwa ajili ya michezo
- Raba rangi nyeupe.
- Bukta na Tshirt rangi ya bluu.

**(b) WAVULANA:**


- Suruali mbili ndefu rangi ya kijivu cha kupauka mbele iwe na rinda na chini iwe na upana wa wastani .(isiwe na mitindo kama vile, Modal, jeans style n.k)
- Shati mbili mikono mifupi (aina ya Tomato)
- Mkanda mweusi wa ngozi
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na visigino virefu na **visiwe** buti.
- Soksi nyeupe ndefu(jozi mbili)
- Sweater 1 kwa ajili ya kujikinga na baridi(Rangi **kijivu**)

**Nguo za kushindia na shamba dress na Michezo**

- Suruali nyeusi mbili na Tshirt mbili cream zenye nembo ya shule(Tshirt zinapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh 15,000/= kwa moja).
- Track suit rangi ya kijivu kwa ajili ya michezo
- Bukta na Tshirt rangi ya bluu
- Raba rangi nyeupe



( HIJABU YA "SHAMBA DRESS")



( HIJABU YA "DARASANI")



(SKETI YA DARASANI



(SURUALI YA DARASANI)



(SWETA MIKONO MIREFU)



(TRAKI SUTI)

## 1.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari yasipungue 15;
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika angalau kimoja kwa kila somo(vilivyotungwa na TIE)
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;
vi. Godoro futi 2½ x6
vii. Sanduku imara la chuma na kufuli imara
viii. Mashuka Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 (*rangi ya bluu bahari);*
ix. Nguo za ndani za kutosha;
x. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
xi. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko
xii. Kwanja 1,Panga 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.(kwa wote)
xiii. Mwanafunzi wa HGK, CBG na PCB aje na hardbroom,
xiv. Mwanafunzi wa HGLna PCM aje na brush za chooni na moper;
xv. Aje na kadi ya Bima ya Afya, kama hana mzazi aandae utaratibu wa kupata bima shuleni;

**MUHIMU: Afike na hati ya matokeo yake ya kidato cha nne (Result slip), Nakala ya cheti cha kuhitimu kidato cha nne (Leaving Certificate) na nakala ya cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate)**

## 1.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Fedha zote zilipwe kupitia akaunti ya shule, NMB 70201200056 MAHIWA SECONDARY SCHOOL**

## 2. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**4.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shu**

**Jina la Mkuu wa Shule :HONORATI EPIMACK TARIMO**

**Mhuri wa Mkuu wa Sh**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MAHIWA
S. L. P. 129 MTAMA LINDI

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa**.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule : 0717404471/0757246378**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0712999822**
- **Mwandamizi Taaluma :0716506630**
- **Mwandamizi Malezi :0682546688/0673446103**

PRESIDENT'S OFFICE,

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

Mahiwa secondary school
P.O.BOX 129
Mtama - Lindi

REF: NO …………………………….
To The Medical Officers(District/regional)
…………………………………………………………
Sir/Madam,

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION TO
(*Name of student)………………………………………………………*

Please examine the above named student and give the report regarding his/her suitability for undertaking secondary school studies.

1. Student's full name………………………………………………………………………………
2. Blood……………………………………………………………………………………………………..
3. Stool……………………………………………………………………………………………………
4. T.B test ……………………………………………………………………………………………….
5. Syphilis test…………………………………………………………………………………………..
6. Urine examination…………………………………………………………………………………..
7. Eyes test ……………………………………………………………………………………………..
8. Chest test……………………………………………………………………………………………..
9. Ears test……………………………………………………………………………………………
10. Spleen…………………………………………………………………………………………………
11. Abdomen……………………………………………………………………………………………
12. Pregnancy (for girls only)………………………………………………………………………

ANY ADDITIONAL INFORMATION: EG Physical defects or impairment,infection, family diseases etc
……………………………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………

COMMENTS:……………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………

I certify that the above student is suitable/unsuitable for secondary school studies. If unsuitable give reasons
……………………………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………

Name of Medical Officer……………………………………………………Signature ………………………
Date……………………………………………………………….. Official stamp ………………………………

## MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI.

1. JINA LA MWANAFUNZI…………………………………………………………………
2. TAREHE YA KUZALIWA………………………………………………………………
3. MAKAZI
   - Mtaa……………………………………………..
   - Kijiji…………………………………………………
   - Kata………………………………………………
   - Tarafa………………………………………………
   - Wilaya…………………………………………………
   - Mkoa…………………………………………………
4. SHULE
   - Shule ya Msingi aliyosoma hadi darasa la saba……………………………….
     na mwaka wa kuhitimu……………………....
   - Shule ya Sekondari aliyosoma hadi kidato cha nne…………………………
     Na mwaka wa kuhitimu…………………………..
5. TAARIFA ZA WAZAZI NA NDUGU WA KARIBU

   A. JINA LA BABA MZAZI/MLEZI……………………………………………..
   - SIMU YA BABA MZAZI/MLEZI………………………………………………
   - MAKAZI……………………………………………………………………

   B. JINA LA MAMA MZAZI/MLEZI………………………………………………
   - SIMU YA MAMA MZAZI/MLEZI………………………………………………
   - MAKAZI……………………………………………………………………

   C. NDUGU WA KARIBU

   1.JINA……………………………………………………………………
   - UHUSIANO…………………………………………………
   - SIMU…………………………MAKAZI……………………..

   2.JINA……………………………………………………………………
   - UHUSIANO…………………………………………………
   - SIMU……………………….MAKAZI……………………………

## A: YAH: KUKUBALI/KUKATAA NAFASI (MWANAFUNZI) NA MKATABA WA UTIIFU.

Mimi ……………………………………………………………………………….. nakiri kopokea barua ya kujiunga na masomo ya kidato cha Tano katika shule ya sekondari mahiwa. Baada ya kusoma na kuelewa yaliyoandikwa katika fomu hii NIMEKUBALI NAFASI/NIMEKATAA NAFASI ya kuendelea na masomo.

Ninaahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu kuwa nitazingatia kanuni, sheria na taratibu zote za shule. Kamwe sitoshiriki au kujihusisha na vitendo vya uvunjaji wa sheria za shule na makosa mengine ya jinai.

Nitatumia juhudi na maarifa katika kujifunza kwa manufaa yangu, wazazi, jamii na taifa kwa ujumla. Aidha niaahidi kuwepo shuleni muda wote na endapo itatokea nataka kutoka nje ya shule nitaomba ruhusa na kuvaa sare rasmi za shule.

Jina la mwanafunzi ……………………………………………saini ……………………..tarehe……………………

Jina la mzazi/mlezi ……………………………………………saini……………………..tarehe……………………

**B. MAKUBALIANO YA MZAZI/MLEZI.**

Mimi ……………………………………………. Mzazi/mlezi wa mwanafunzi ……………………………..
Wa kidato cha …………….. mwaka …………………….. ninakubaliana na masharti tajwa hapo juu, hivyo naahidi kutekeleza mkataba huu na kuamuru mwanangu autekeleze. Endapo mwanangu atashindwa kutekeleza basi sheria ifuate mkondo wake.

Jina la mzazi…………………………………………

Sahihi ya mzazi/mlezi………………………………..

Tarehe…………………………………………………

## VITABU ZIADA VINGINE VINAVYOPENDEKEZWA

| S/N | JINA LA KITABU | MWANDISHI | SOMO |
|---|---|---|---|
| 01 | Advanced Level Literature Forms 5& 6 | Nyambari Nyangwine | English 2 |
| 02 | Advanced level English | Nicholas Asheli | English 1 |
| 03. | Advanced Level Language | Oxford | English 1&2 |
| 04 | Nadharia ya Lugha | Nyambari Nyangwine | Kiswahili 1 |
| 05 | Nadharia ya Fasihi | Nyambari Nyangwine | Kiswahili 2 |
| 06 | TAHAKIKI kidato cha 5&6 | Nyambari Nyangwine | Kiswahili 2 |
| 07 | Physical Geography | Zisti Kamili | Geography 1 |
| 08 | Practical Geography | Zisti Kamili | Geography 1 |
| 09 | Human and Economic Geography | Msabili D.T. | Geography 2 |
| 10 | General Studies Notes forms 5&6 | Nyambari Nyangwine | General studies |
| 11 | Essentials in Advanced level History paper 2 | Salehe Yasini | History 2 |
| 12 | Essentials in Advanced level History paper 1 | Salehe Yasini | History 1 |
| 13 | History lesson notes for advanced level paper 1 &2 | Bakari Madaya | History 1&2 |

**English language**

1. Advanced level English language 1 form 5 & 6. Shadrack G.Ndambo
2. The real English textbook for advanced level. Dr. Kadeghe Michael
3. Advanced English Language 1 form 5 and 6. Oxford
4. English language paper 2. Nicholous Asheli
5. English language paper 2. Nyambari Nyangwine
6. Advanced Level English Language Structure & Stylistics. Nicholous Asheli
7. The Comprehensive Linguistics. Mgonja, M.E
8. Linguistics Concepts for Advanced Learners. Julton Sanga

**Readings**

1. A Man of the People. Chinua Achebe
2. The Beautiful Ones Are Not Yet Born. Ayi Kwei Armah
3. His Excellency the Head of State. Danny Sado
4. Betrayal in the City. Francis Imbuga
5. Black Mamb John Ruganda
6. Lwanda Magere. Okoiti
7. The Bride Austin Bukenya
8. The woundrful surgen and the poems by Charles Mloka
9. I Will Marry When I Want. Ngugi wa Thiongo & Ngugi wa Mirii
10. An Enemy of the People. Henrisk Ibsen
11. Selected Poem. Institute of Education
12. The wonderful Surgeon and other Poems. Charles Mloka
13. Encounters from Africa by macxmillian educ .Ltd
14. Vanishing shadows by Namige Kyando
15. A season of waiting by david omewale
16. Rape of the peart by

**KISWAHILI**
Kiswahili kidato cha V na VI (oxford)
Kiswahili kidato cha V na VI (TIE)
Kiswahili kidato cha V na VI (saluhayo)

A. **RIWAYA**
1. Vuta Nkuvute
2. Mfadhili
3. Usiku Utakapo Kwisha
4. Kufikilika

B. **TAMTHILIYA**
1. Morani
2. Kivuli kinaishi
3. Nguzo mama
4. Kwenye ukingi wa thim

C. **USHAIRI**
1. Fungate la Uhuru
2. Kimbunga
3. Mapenzi Bora
4. Chungu Tamu